BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2014

# KISWAHILI

# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2014

# KISWAHILI

Kimechapishwa na

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2014

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO


DIBAJI .................... iv

1.0. UTANGULIZI .................... 1

2.0. UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA .................... 1

- 2.1 Sehemu A. Sarufi .................... 1
- 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi .................... 20
- 2.3 Sehemu C: Ufahamu .................... 30
- 2.4 Sehemu D: Ushairi .................... 40
- 2.5 Sehemu E: Utungaji .................... 47

3.0. HITIMISHO .................... 48

4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO .................... 50

**KIAMBATISHO A** .................... 52

# DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa somo la Kiswahili imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watunga sera, wakaguzi, watunga mitalaa na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya mtihani huo. Majibu ya wanafunzi katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi waliweza kujifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya elimu ya msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya wanafunzi kutoweza kujibu maswali kwa usahihi: kushindwa kutambua matakwa ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo; kutofahamu kanuni za lugha na matumizi ya misamiati; kutojibu kabisa baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja kinyume na maelekezo katika mtihani. Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya watahiniwa waliojibu maswali kwa usahihi, walioshindwa kuchagua jibu sahihi, walioacha kujibu swali na ambao waliandika jibu zaidi ya moja katika swali husika.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupatia ufumbuzi dosari zilizoainishwa katika taarifa hii.

Aidha, Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa watakayopata wanafunzi wanaohitimu elimu ya msingi vitaongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kitaongezeka pia.

Mwisho Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Maafisa wa Mifumo, Makatibu Muhtasi na wafanyakazi wa idara ya Chapa na Uchapishaji na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatasaidia katika kuboresha taarifa ya uchambuzi wa maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa siku zijazo.

Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kuhusu namna ambavyo watahiniwa walijibu maswali katika mtihani wa somo la Kiswahili. Mtihani wa Kiswahili ulikuwa na maswali **50** ya kuchagua jibu sahihi ambayo yalikuwa yamegawanyika katika sehemu tano kama ifuatavyo: Sehemu A: Sarufi; B: Lugha ya Kifasihi; C: Ufahamu: D: Ushairi na E: Utungaji. Jumla ya watahiniwa **808,085** walisajiliwa kufanya mtihani wa **PSLE 2014** ambapo miongoni mwao waliofanya mtihani wa somo la Kiswahili walikuwa **791,924** na kati yao watahiniwa **552,003** sawa na asilimia **69.70** walifaulu mtihani huo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa kwa kila swali umefanyika. Sehemu hii inaainisha maswali yaliyoulizwa na majibu ya kuchagua waliyopewa. Idadi ya watahiniwa waliochagua kila jibu na asilimia yao imeoneshwa. Aidha, uchambuzi wa sababu zinazoweza kuwa zilichangia kuwafanya wasichague jibu sahihi zimeainishwa.

### 2.1 Sehemu A. Sarufi

**Swali la 1**: Yeye amefaulu mitihani yake vizuri." Katika sentensi hii neno lipi limetumika kama kielezi?

A. Amefaulu

B. Yeye

C. Vizuri

D. Mitihani

E. Yake.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 164,597 | 254,377 | 268,857 | 69,308 | 31,632 | 1,577 | 1,584 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 20.78 | 32.12 | 33.95 | 8.75 | 3.99 | 0.2 | 0.2 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno. Asilimia 33.95 sawa na watahiniwa 268,857 walichagua jibu C "Vizuri" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 164,597 sawa na asilimia 20.78 walichagua kipotoshi A "amefaulu" ambacho ni kitenzi. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa tofauti ya kielezi na kitenzi hivyo kushindwa kutambua kuwa kielezi ni neno linalofafanua zaidi taarifa kuhusu kitenzi. Aidha, kipotoshi B "Yeye" ambacho sio jibu sahihi kilichaguliwa na watahiniwa 254,377 sawa na asilimia 32.12 ambacho ni Kiwakilishi. Hata hivyo kwa kanuni ya lugha ya Kiswahili kielezi hakiwezi kuwa mwanzoni mwa sentensi hiyo aliyopewa. Hali kadhalika kuwepo kwa watahiniwa 69,308 sawa na asilimia 8.75 waliochagua kipotoshi D "Mitihani" ambacho sio jibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kujua kuwa neno "mitihani" pamoja na kufuata baada ya kitenzi sio kielezi bali ni nomino kwa sababu halitoi taarifa ya namna alivyofaulu bali limeeleza kipi alichofaulu. Hali kadhalika, watahiniwa 31,632 sawa na asilimia 3.99 walichagua kipotoshi E "Yake" ambacho sio jibu sahihi kwa sababu chaguo hilo ni kivumishi kimilikishi kinachoelezea habari zaidi kuhusu nomino "mitihani" hivyo hakiwezi kuwa kielezi.

**Swali la 2:** "Dada ameandika barua kwa baba." Sentensi hii iko katika kauli gani?

A Kutendea

B Kutenda

C Kutendwa

D Kutendeana

E Kutendeka.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 107,555 | 347,855 | 83,527 | 55,184 | 194,572 | 1,539 | 1,700 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 13.58 | 43.92 | 10.55 | 6.97 | 24.57 | 0.19 | 0.21 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kutambua kauli za vitenzi. Watahiniwa 347,855 sawa na asilimia 43.92 walichagua jibu B "Kutenda" ambalo ni jibu sahihi. Sababu iliyowafanya watahiniwa kupata swali hili kwa usahihi ni uwezo wa kuhusisha tabia ya kitenzi cha Kiswahili ambacho kikiwa katika hali ya uyakinishi hukamilishwa na kiambishi tamati maana -a- kuonesha utendaji wa jambo. Watahiniwa waliochagua kipotoshi A "Kutendea" walishindwa kulitambua umbo la -e- ambalo ni la kauli ya kutendea. Aidha, watahiniwa waliochagua kati ya vipotoshi C, D na E ambao ni 194,572 sawa na asilimia 42.09 walishindwa kugundua upungufu uliokuwepo katika vipotoshi hivyo ambapo maumbo -w-, -an- na -ean- hayajipambanui na kauli ya kutenda bali ya kutendwa, kutendeka na kutendeana.

**Swali la 3**: Katika sentensi zifuatazo ipi ni sahihi?

A. Nimekuja hapa tangia asubuhi

B. Nimekuja hapa tangiapo asubuhi

C. Nimekuja hapa tanguapo asubuhi

D. Nimekuja hapa tangu asubuhi

E. Nimekuja hapa tangiepo asubuhi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 124,616 | 32,323 | 31,772 | 577,930 | 21,788 | 1,808 | 1,695 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.74 | 4.08 | 4.01 | 72.98 | 2.75 | 0.23 | 0.21 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika utumizi wa lugha. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi (577,930) sawa na asilimia 72.98 ambao walichagua D "Nimekuja hapa tangu asubuhi" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 124,616 sawa na asilimia 15.74 walichagua kipotoshi A "Nimekuja hapa tangia asubuhi" ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walivutwa na lugha ya mazungumzo isiyo sanifu ya kutumia neno tangia badala ya tangu. Aidha, watahiniwa 85,883 sawa na asilimia 11.56 walichagua kati ya kipotoshi B, "Nimekuja hapa tangiapo asubuhi," C "Nimekuja tanguapo asubuhi' na E "Nimekuja hapa tangiepo asubuhi," ambavyo sio majibu sahihi jambo linaloonesha kuwa walikosa maarifa ya semantiki ya Kiswahili. Watahiniwa hao walivutiwa na maneno "tanguapo," "tangiapo" na "tangiepo" bila kutambua kuwa kisarufi hayakuwa maneno sahihi. Athari za kimatamshi zinaweza pia kuwa zilichangia kwa watahiniwa waliochagua vipotoshi B, C na E.

**Swali la 4:** Neno lipi ni **tofauti** na maneno mengine kati ya maneno yafuatayo?

A. Viwakilishi

B. Vivumishi

C. Vielezi

D. Vitenzi

E. Visaidizi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 41,125 | 47,927 | 47,208 | 40,302 | 615,386 | 2,522 | 2,462 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.19 | 5.42 | 5.96 | 5.09 | 77.71 | 0.32 | 0.31 |

Swali hili lilipima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi (615,386), kwani asilimia 77.71 walijibu swali hili vizuri kwa kuchagua jibu E "Visaidizi" ambalo ndilo jibu sahihi kwa kuwa visaidizi sio aina ya neno bali ni aina ya vitenzi. Watahiniwa 176,562 ambao ni asilimia ndogo (16.47) ndiyo waliojibu kati ya vipotoshi A "Viwakilishi" B "Vivumishi," C "Vielezi" na D "Vitenzi" ambavyo sio majibu sahihi bali vyote ni aina za maneno yenye mfanano. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa swali lilihusu tofauti na wala sio mfanano.

**Swali la 5**: Tunu angalisoma _______ mtihani wake." Neno lipi linakamilisha sentensi hiyo kwa usahihi?

A. angefaulu

B. angalifaulu

C. asingefeli

D. angelifaulu

E. asingalifaulu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 128,259 | 501,343 | 44,531 | 92,085 | 22,306 | 1,441 | 1,967 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 16.2 | 63.31 | 5.62 | 11.63 | 2.82 | 0.18 | 0.25 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kutumia maneno katika sentensi zenye hali ya masharti. Watahiniwa 501,343 sawa na asilimia 63.31 walikuwa na uelewa wa swali hili kwani walichagua jibu B "angalifaulu" ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi A "angefaulu" na D "angelifaulu" vilivyochaguliwa na watahiniwa 220,344 ambao ni sawa na asilimia 27.83 unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masharti ya umbo la "ngali" kufuatiwa na umbo la –ngali- katika kuikamilisha sentensi yakinishi. Uchaguzi wa kati ya kipotoshi C "asingefeli" na E "asingalifaulu" vilivyochaguliwa na watahiniwa 66,837 ambao ni sawa na asilimia ndogo (8.44) unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa sentensi hiyo ni yakinishi na haiwezi kukamilishwa na umbo la "singali," "singe" ambayo yote ni maumbo yanaonesha ukanushi.

**Swali la 6**: "Mnyama mkali amekamatwa leo." Katika sentensi hii neno "mkali" limetumika kama aina gani ya neno?

A. Kielezi
B. Kiwakilishi
C. Kitenzi
D. Kivumishi
E. Kiunganishi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 176,899 | 124,152 | 79,717 | 341,158 | 65,099 | 2,613 | 2,294 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 22.34 | 15.68 | 10.07 | 43.08 | 8.22 | 0.33 | 0.29 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua aina za maneno. Watahiniwa 341,158 sawa na asilimia 43.08 walichagua jibu D "Kivumishi" ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 22.34 ambayo inawakilisha watahiniwa 176,899 walichagua kipotoshi A "kielezi" ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walivutiwa na maana ya kielezi kuwa ni kutoa taarifa na wakashindwa kuelewa kuwa neno linalofuata baada ya nomino linatoa taarifa kuhusu nomino hivyo haliwezi kuwa kielezi bali ni kivumishi. Aidha, katika kanuni ya lugha ya Kiswahili nomino haiwezi kufuatwa na kielezi. Hali kadhalika kuwepo kwa watahiniwa 268,968 sawa na asilimia 33.97 ya watahiniwa waliochagua kati ya kipotoshi B, "Kiwakilishi", C "Kitenzi" na E "Kiunganishi" kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kwa muundo wa kawaida wa lugha ya Kiswahili kiwakilishi hakiwezi kufuatana na nomino inayowakilishwa bali hutokea katika mazingira maalum kama vile viapo na mikataba. Pia vitenzi viwili vikuu haviwezi kufuatana katika sentensi sahili. Aidha, watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa katika sintaksia ya lugha

ya Kiswahili huwezi kutumia kiunganishi kuunganisha nomino na kitenzi.

**Swali la 7**: "Juma amefika na hatacheza mpira." Kitenzi "hatacheza" kipo katika hali gani?

A. Ukanushi

B. Timilifu

C. Mazoea

D. Ujao

E. Shurutia.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 278,635 | 149,296 | 96,324 | 206,546 | 56,446 | 2,464 | 2,221 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 35.18 | 18.85 | 12.16 | 26.08 | 7.13 | 0.31 | 0.28 |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kutambua hali za vitenzi. Watahiniwa 278,635 sawa na asilimia 35.18 walichagua chaguo A "Ukanushi" ambalo ndilo jibu sahihi kutokana na kiambishi awali -ha- kuwa katika hali ya ukanushi. Watahiniwa 206,546 sawa na asilimia 26.08 waliochagua kipotoshi D "Ujao" ambacho sio jibu sahihi huenda walivutiwa na kiambishi -ta- kinachoonesha wakati ujao. Hata hivyo walishindwa kuelewa kuwa swali lilihusu hali za vitenzi na sio njeo za nyakati. Watahiniwa 245,620 sawa na asilimia 38.14 walichagua kati ya kipotoshi B "Timilifu" na C, "Mazoea" ambavyo vyote sio majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa hali timilifu inawakilishwa na kiambishi -me- na hali ya mazoea inawakilishwa na kiambishi -hu- ambavyo vyote havikuwepo katika kitenzi "hatacheza." Aidha, asilimia ndogo (7.13) ambayo ni watahiniwa 56,446 waliochagua kipotoshi E "Shurutia" ambacho pia

sio jibu sahihi, walishindwa kutambua kuwa kitenzi hicho hakikuwa na umbo lolote la masharti kama vile -ki-, -nge-, ngali na -ngeli-.

**Swali la 8:** "Alisema hanywi dawa tena." Kauli halisi ya sentensi hii ni ipi?

A. "Hanywi dawa"

B. "Hatakunywa dawa"

C. "Sinywi dawa"

D. "Sitakunywa tena dawa"

E. "Sinywi tena."

Majibu ya watahihiwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 93,555 | 112,009 | 189,561 | 351,158 | 41,292 | 2,305 | 2,052 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.81 | 14.14 | 23.94 | 44.34 | 5.21 | 0.29 | 0.26 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa watahiniwa katika kuelewa kauli za sentensi na lilimtaka mtahiniwa kuonesha kauli halisi ya sentensi "Alisema hanywi dawa tena." Watahiniwa 189,561 sawa na asilimia 23.94 walichagua jibu C "Sinywi dawa" ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi huo unaonesha kuwa watahiniwa walielewa kuwa kauli halisi inayohitajika ni ile ya wakati uliopo kutokana na kauli taarifa iliyopo katika swali kuwa katika wakati huo. Kuwepo kwa jumla ya watahiniwa 351,158 sawa na asilimia 44.34 waliochagua kipotoshi D "Sitakunywa tena dawa" kunaonesha wazi kuwa watahiniwa walikosa ujuzi unaohusu njeo za nyakati katika sentensi kwa vile kipotoshi hicho kipo katika njeo ya wakati ujao. Aidha, watahiniwa 205,564 sawa na asilimia 25.95 waliochagua kati ya kipotoshi A "Hanywi dawa" na B "Hatakunywa dawa" walishindwa kutambua kuwa hizo sio kauli halisi bali ni kauli taarifa ambazo hazikukamilika. Watahiniwa wachache, (42,292) sawa na asilimia ndogo (5.21) waliochagua

kipotoshi E “Sinywi dawa” ambacho sio jibu sahihi walishindwa pia kuelewa kuwa sentensi hiyo pamoja na kuwa kauli halisi haijataja kile kisichonywewa ambacho ni dawa hivyo kupoteza mantiki ya swali.

**Swali la 9**: “Walikotoka kuna mvua.” Sentensi hiyo ipo katika wakati gani?

A. Mazoea
B. Shurutia
C. Uliopo
D. Uliopita
E. Ujao.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 47,690 | 52,005 | 201,945 | 453,257 | 32,567 | 2,570 | 1,898 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 6.02 | 6.57 | 25.5 | 57.23 | 4.11 | 0.32 | 0.24 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua njeo za nyakati. Watahiniwa 453,257 sawa na asilimia 57.23 walichagua jibu D “Uliopita” ambalo ndilo jibu sahihi. Asilimia 25.5 ambayo inawakilisha watahiniwa 201,945 walichagua kipotoshi C “Uliopo” ambacho sio jibu sahihi. Watahiniwa hao walivutiwa na neno “kuna” ambalo ni kitenzi kishirikishi ambacho katika kanuni za Kiswahili hakibebi dhana ya wakati kwa vile dhana hiyo inabebwa kwenye kitenzi kikuu “Toka.” Kuwepo kwa watahiniwa 80,257 sawa na asilimia 10.13 waliochagua kati ya kipotoshi A na E kunaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha wa kutambua viambishi vya njeo za nyakati kwa vile kitenzi “walipotoka” kina kiambishi -li- ambacho ni cha wakati uliopita. Aidha, wakati wa mazoea hutambulishwa na kiambishi -hu-, na wakati ujao

huwakilishwa na kiambishi –ta- hivyo kufanya vipotoshi hivyo kutokuwa majibu sahihi. Watahiniwa 32,567 ambao ni sawa na asilimia 4.11 walichagua kipotoshi “Shurutia” ambacho sio jibu sahihi kwa sababu shurutia sio wakati bali ni tungo ambayo huwa na maumbo yake kama -ki-, –nge-, -ngali- na –ngeli- ambayo hujenga tungo shurutia.

**Swali la 10:** “Hamisa na Hanifa ni mapacha walioungana.” Katika sentensi hii neno “na” limetumika kama aina gani ya neno?

A. Kihisishi
B. Kiunganishi
C. Kimilikishi
D. Kivumishi
E. Kiwakilishi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 45,765 | 571,927 | 44,120 | 54,692 | 71,160 | 2,064 | 2,204 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.78 | 72.22 | 5.57 | 6.91 | 8.99 | 0.26 | 0.28 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi (571,927) ambao ni sawa na asilimia 72.22 waliochagua B ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 215,737 sawa na asilimia 27.25 walichagua kati ya kipotoshi A “Kihisishi,” C “Kimilikishi,” D “Kivumishi” na E “Kiwakilishi” ambayo yote sio majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa maneno yote hayo hayawezi kukaa katikati ya nomino mbili na kupata maana ya sentensi iliyokusudiwa kwa sababu kwa kanuni ya sintakisia ya lugha ya Kiswahili jambo hilo haliwezekani.

**Swali la 11:** Panya huyu anakula unga wangu. Wingi wa sentensi hii ni upi?

A. Panya hawa wanakula unga wangu

B. Mapanya hawa wanakula unga wetu

C. Panya hizi zinakula unga wangu

D. Panya hizi zinakula unga wetu

E. Panya hawa wanakula unga wetu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 298,079 | 87,471 | 44,926 | 41,563 | 315,117 | 1,777 | 2,.999 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 37.64 | 11.05 | 5.67 | 5.25 | 39.79 | 0.22 | 0.38 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutumia maneno katika umoja na wingi. Watahiniwa 315,117 yaani asilimia 39.79 walikuwa na uelewa wa swali hili kwani walichagua jibu E “Panya hawa wanakula unga wetu” ambalo ni jibu sahihi. Watahiniwa 298,079 sawa na asilimia 37.64 waliochagua kipotoshi A, “Panya hawa wanakula unga wangu” huenda walivutiwa na mwanzo wa sentensi hiyo “Panya hawa wanakula unga wangu” ambayo ilionekana kukidhi ruwaza ya swali lakini wakasahau kuwa kimilikishi “wangu” kilikuwa katika umoja na kilipaswa kubadilishwa na kuwa katika wingi. Uchaguzi wa kipotoshi B “Mapanya hawa wanakula unga wetu” kwa watahiniwa 87,471 ambao ni sawa na asilimia 11.05 unaonesha kuwa watahiniwa hao waliathiriwa na tabia ya baadhi ya nomino ambazo zina uwezo wa kupokea umbo la wingi kwa mfano mnyama (umoja) na wingi (wanyama) bila kujua kuwa majina mengi ya wanyama hayana umoja na wingi. Aidha, watahiniwa 86,489 ambao ni sawa na asilimia 10.92 waliochagua kati ya kipotoshi C na D walishindwa kutambua kuwa jina “Panya” ni mojawapo ya majina ya wanyama ambayo umoja na wingi

wake unafanana. Hivyo kwa kukosa ujuzi huo watahiniwa hao walishindwa kutoa jibu lililo sahihi kwa vile walivutiwa na vipotoshi vyenye maneno “hizi” kuwa ndivyo vimejenga wingi wa tungo hizo. Hali hii inadhihirisha kuwa watahiniwa wengi hawana uelewa wa kutosha kuhusu umbo mahsusi lioneshalo wingi katika sentensi.

**Swali la 12**: Siku ile ya maandamano kulikuwa na __________wa pikipiki. Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo?

A. msururu

B. msuluru

C. msurulu

D. mslululu

E. musururu

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 364,842 | 71,537 | 81,982 | 219,915 | 48,611 | 2,499 | 2,546 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 46.07 | 9.03 | 10.35 | 27.77 | 6.14 | 0.32 | 0.32 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika matumizi ya msamiati na usanifu wa lugha. Watahiniwa 364,842 ambao ni sawa na asilimia 46.07 walichagua A “msururu” ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi D kwa watahiniwa 219,915 sawa na asilimia 27.77 umetokana na watahiniwa kuathiriwa na matamshi yanayotokana na athari ya lugha ya asili ambapo walishindwa kutofautisha sauti -r- na -l-. Aidha, uchaguzi wa vipotoshi B, C  na E kwa watahiniwa 202,130 ambao ni sawa na asilimia 25.52 unadhihirisha kuwa, watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu usanifu wa lugha kwa sababu

maneno “msuluru,” “msurulu” na “musururu” sio maneno sanifu ya Kiswahili bali hutumiwa kutokana na athari ya matamshi.

**Swali la 14:** Neno mchwa lina silabi ngapi?

A. Mbili

B. Tano

C. Moja

D. Nne

E. Tatu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 418,407 | 120,051 | 122,684 | 55,699 | 70,086 | 2,577 | 2,428 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 52.83 | 15.16 | 15.49 | 7.03 | 8.85 | 0.33 | 0.31 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika sarufi ya lugha. Watahiniwa 418,407 sawa na asilimia 52.83 walichagua A “Mbili” ambalo ni jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi B “Tano,” C “Moja,” D “Nne” na E “Tatu” kwa watahiniwa 368,520 ambao ni sawa na asilimia 46.53 unadhihirisha kuwa, watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu utambuzi wa silabi katika uundaji wa maneno ya Kiswahili.

**Swali la 15**:“Hapa ________alipoishi chifu Mirambo.” Ni neno lipi linakamilisha sentensi hiyo kwa usahihi?

A. ndiko

B. ndimo

C. ndiyo

D. ndipo

E. ndio

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 60,323 | 51,864 | 80,263 | 538,733 | 56,273 | 2,175 | 2,301 |
| Asilimia ya watahiniwa | 7.62 | 6.55 | 10.14 | 68.03 | 7.11 | 0.27 | 0.29 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika sarufi ya lugha. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi (538,733) sawa na asilimia 68.03 walichagua D "ndipo" ambalo ni jibu sahihi kwa sababu ya umbo –po- ambalo huonesha mahali chifu alipoishi kutokana na upatanisho wa kisarufi unaojionesha wazi katika kitenzi "alipoishi." Uchaguzi wa vipotoshi A "ndiko," B "ndimo," C "ndiyo" na E "ndio" kwa watahiniwa 248,723 ambao ni sawa na asilimia 31.42 unadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu muundo wa sentensi katika kuangalia upatanisho wa kisarufi.

**Swali la 16:** Atakapomnyonyoa yule bata____________kwenye moto.

A. atambanika

B. anambanika

C. humbanika

D. amembanika

E. alimbanika

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 605,370 | 55,048 | 44,135 | 39,230 | 44,111 | 1,941 | 2,097 |
| Asilimia ya watahiniwa | 76.44 | 6.95 | 5.57 | 4.95 | 5.57 | 0.25 | 0.26 |

Swali hili lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutumia njeo ya wakati. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi

na watahiniwa wengi (605,370) sawa na asilimia 76.44 walijibu swali hili vizuri kwa kulichagua chaguo A “atambanika” ambalo ndilo jibu sahihi. Aidha, watahiniwa 182,524 ambao ni sawa na asilimia 23.04 walichagua kati ya vipotoshi B “anambanika,” C “humbanika” D “amembanika” na E “alimbanika” ambavyo sio majibu sahihi kwani walishindwa kutambua kuwa umbo la wakati ujao -ta- lililokuwa kwenye kitenzi “atakapomnyonyoa” linakwenda sambamba na umbo -ta- kwenye jibu sahihi “atambanika.” Aidha, maumbo ya -na-, -hu-, me- na -li- katika vipotoshi hivyo yanaonesha njeo za wakati uliopo, mazoea, timilifu na uliopita tofauti na umbo la wakati lililopo kwenye shina la swali “Atakapomnyonyoa.”

**Swali la 17**: “Kitabu changu ni cheusi, chako ni cheupe.” Neno “chako” ni aina gani ya neno?

A. Kivumishi

B. Kiwakilishi

C. Kielezi

D. Kihusishi

E. Kiunganishi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 151,977 | 273,258 | 191,717 | 70,030 | 100,616 | 2,319 | 2,015 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 19.19 | 34.51 | 24.21 | 8.84 | 12.71 | 0.29 | 0.25 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za maneno. Watahiniwa 273,258 sawa na asilimia 34.51 walichagua jibu B “Kiwakilishi” ambalo ndilo jibu sahihi. Aidha, watahiniwa 151,977 waliochagua kipotoshi A “Kivumishi” walishindwa kuelewa kuwa nomino isipotajwa huwa inawakilishwa na kiwakilishi na kivumishi

hakiwezi kuwepo bila ya kutanguliwa na nomino au kiwakilishi. Hata hivyo, watahiniwa hao huenda walivutwa na neno cheusi kwa kulitambua kama nomino wakati neno hilo ni kivumishi. Hali kadhalika, kuwepo kwa watahiniwa 362,363 sawa na asilimia 45.76 waliochagua kati ya kipotoshi C, D na E yaani “Kielezi,” “Kihusishi” na “Kiunganishi” kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kwa muundo wa sentensi waliyopewa kielezi hakiwezi kuanza mwanzoni mwa tungo na kihusishi huwa kinahusisha nomino na nomino au kiwakilishi na kiwakilishi au kiwakilishi na nomino. Aidha, watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa kiunganishi hakiwezi kuunganisha kielezi na kitenzi kisaidizi.

**Swali la 18:** Yeye ni kijana mdogo. Neno “yeye” lipo katika nafsi gani?

A. Ya kwanza umoja
B. Ya tatu umoja
C. Ya pili umoja
D. Ya tatu wingi
E. Ya pili wingi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 224,340 | 249,597 | 186,685 | 56,269 | 71,583 | 1,690 | 1,768 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 28.33 | 31.52 | 23.57 | 7.11 | 9.04 | 0.21 | 0.22 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua matumizi ya nafsi katika tungo. Watahiniwa 249,597 sawa na asilimia 31.52 walichagua jibu B “Ya tatu umoja” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi A “Ya kwanza umoja” ambacho sio jibu sahihi kwa watahiniwa 224,340 ambao ni sawa na asilimia 28.33 unaonesha kuwa watahiniwa wengi hawana ujuzi wa mada ya kutambulisha watu wengine kwa vile “Ya kwanza umoja” ni “Mimi” na sio “Yeye.” Hali

kadhalika kuwepo kwa watahiniwa 314,537 sawa na asilimia 39.72 waliochagua kati ya kipotoshi C, D na E yaani “Ya pili umoja,” “Ya pili wingi” na “Ya tatu wingi” inaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa na ujuzi wa kutambua umoja na wingi katika tungo.

**Swali la 19**: Kinyume cha kitenzi “paa” ni kipi?

A. Toweka
B. Potea
C. Elea
D. Shuka
E. Tua.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 65,116 | 94,839 | 85,862 | 144,093 | 397,642 | 1,986 | 2,394 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.22 | 11.98 | 10.84 | 18.2 | 50.21 | 0.25 | 0.3 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa kuhusu matumizi ya msamiati unaoonesha kinyume cha maneno katika lugha. Watahiniwa 397,642 ambao ni sawa na asilimia 50.21 walichagua E “Tua” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa vipotoshi A “Toweka” na B ”Potea” kwa watahiniwa 159,955 ambayo ni sawa na asilimia 20.2 ambavyo sio majibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa vipotoshi hivyo vina maana sawa. Aidha, kuwepo kwa watahiniwa 229,955 sawa na asilimia 29.04 waliochagua kati ya kipotoshi C na D ambavyo sio sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao hawajua maana ya “Elea” ambayo maana yake ni kuwa juu ya maji bila ya kuzama na “Shuka” maana yake ni kwenda chini au kuteremka kutoka juu ya kitu kwa mfano mti, mlima au gari. Hivyo, kwa kuzingatia maana hizo, inayafanya  maneno hayo yawe tofauti kimaana na neno “paa.”

**Swali la 20:** Mwalimu J.K. Nyerere ni mwasisi wa chama cha TANU. Neno “ni” limetumika kama aina ipi ya kitenzi?

A. Kitenzi kikuu

B. Kitenzi kisaidizi

C. Kitenzi kishirikishi

D. Kitenzi kikamilifu

E. Kitenzi kitegemezi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 156,245 | 258,167 | 252,739 | 57,841 | 61,751 | 2,883 | 2,306 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 19.73 | 32.6 | 31.91 | 7.3 | 7.8 | 0.36 | 0.29 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kutambua aina za vitenzi. Watahiniwa 252,739 sawa na asilimia 31.91 walichagua jibu C “Kitenzi kishirikishi” ambalo ndilo jibu sahihi. Uchaguzi wa kipotoshi B kwa watahiniwa 258,167 sawa na asilimia 32.6 ambacho sio jibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ujuzi wa kutambua umbo linalojenga kitenzi kisaidizi ambalo huwa linabeba kiambishi nafsi na njeo ya wakati ambapo neno -ni- halina umbo hilo. Kuwepo kwa watahiniwa 156,245 ambao ni sawa na asilimia 19.73 waliochagua kipotoshi A “Kitenzi kikuu” ambacho sio jibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kitenzi kikuu hubeba kiambishi nafsi, njeo ya wakati na shina la kitenzi lenye kubeba maana. Aidha, watahiniwa 119,592 sawa na asilimia 15.1 waliochagua kati ya kipotoshi D “Kitenzi kikamilifu” na E “Kitenzi kitegemezi” ambavyo vyote sio majibu sahihi, kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa hakuna aina ya vitenzi vyenye majina kama hayo.

## 2.2 Sehemu B: Lugha ya Kifasihi

**Swali la 21:** "Ulichokitupa pwani____________." Kifungu kipi cha maneno hukamilisha methali hiyo?

A. kakingoje ufuoni
B. kisubiri bandarini
C. utakipata bara
D. hukomea kivukoni
E. hutokomea baharini.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 270,528 | 146,707 | 109,077 | 108,569 | 149,898 | 4,318 | 2,835 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 34.16 | 18.53 | 13.77 | 13.71 | 18.93 | 0.55 | 0.36 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu kutambua muundo wa methali na hasa ukamilishaji wa methali aliyopewa. Watahiniwa 270,528 sawa na asilimia 34.16 walichagua A "kakingoje ufuoni" ambalo ndilo jibu sahihi ikiwa na maana kuwa kitu kikishatupwa pwani inabidi kikasubiriwe ufuoni ambapo ni mahali maji ya bahari hukomea kwa sababu kingeweza kuletwa huko na mawimbi ya bahari. Uchaguzi wa vipotoshi B "kisubiri bandarini" na C "Utakipata bara" ambavyo sio majibu sahihi, vilivyochaguliwa na watahiniwa 255,784 sawa na asilimia 32.3 unaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kujua kuwa kinachosubiriwa bandarini au bara huwa ni mizigo ambayo huletwa kwa utaratibu maalumu na kupokelewa hivyo haiwezekani kiwe kimetupwa. Watahiniwa 258,467 sawa na asilimia 32.64 waliochagua kati ya kipotoshi D "hutokomea kivukoni" na E "hutokomea baharini" ambavyo vyote sio majibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa kitu

kikitokomea maana yake ni kwamba kimetoweka kabisa na hakiwezi kupatikana tena hivyo haiwezekani kikasubiriwa.

**Swali la 22:** "Mkiweza ___________ katika kazi hiyo, hatimaye mtafanikiwa." Nahau ipi inakamilisha tungo hiyo?

A. kuuma na kupulizia

B. kujikaza kisabuni

C. kuwa chuma

D. kuwa na sauti

E. kuwa na nafasi

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 78, 462 | 502,180 | 57, 609 | 56, 915 | 91, 745 | 2,329 | 2,692 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.91 | 63.41 | 7.27 | 7.19 | 11.58 | 0.29 | 0.34 |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kuhusu matumizi ya semi katika lugha ya Kiswahili. Watahiniwa 502,180 sawa na asilimia 63.41 walichagua jibu B "kujikaza kisabuni" ambalo ni jibu sahihi likiwa na maana ya ile hali ya kuvumilia na kustahimili jambo katika hali yoyote. Kwa hiyo, hali hiyo imelinganishwa na jinsi sabuni inavyotumika hadi imalizike kabisa hata kile kichelema. Uteuzi wa kipotoshi A "kuuma na kupulizia" kwa asilimia 9.91 ulifanywa na watahiniwa 78,462 ambao sio jibu sahihi. Watahiniwa hao hakuelewa maana ya msemo huo kuwa ni ile hali ya kujionesha kuwa unafanya jambo kwa nia njema lakini ndani yake nia yake sio nzuri. Aidha, uteuzi wa vipotoshi kati ya C, D, na E kwa asilimia 26.04 vilivyochaguliwa na watahiniwa 206,269 unaonesha ni kwa kwa kiasi gani watahiniwa hawakuwa na ujuzi wa kutosha kuhusu semi mbalimbali za Kiswahili. Kwa mfano uteuzi wa

kipotoshi C “kuwa chuma” ikiwa na maana kutokupenda mabadiliko,” vipotoshi D “kuwa na nafasi” na E “kuwa na sauti” ni misemo ambayo haioneshi bidii yoyote katika kufanya jambo bali inahusiana na utafutaji wa uongozi au kuwa msemaji katika kusimamia jambo. Hivyo misemo hiyo haiwezi kuwa majibu sahihi ya kukamilisha sentensi hiyo ambayo inahitaji msemo uoneshao uvumilivu wa hali ya juu katika kukamilisha jambo.

**Swali la 23:** Methali isemayo, “Ngoma ikilia sana hupasuka” hulingana kimaana na methali ipi kati ya hizi zifuatazo?

A. Mgema akisifiwa tembo hulitia maji

B. Debe tupu haliachi kutika

C. Tamaa mbele mauti nyuma

D. Mpanda ovyo ndiye mla ovyo

E. Mshindo mkuu huvuma mbali.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A*** | **B** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 343,108 | 84,266 | 121,155 | 93,392 | 144,220 | 2,569 | 3,222 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 43.33 | 10.64 | 15.3 | 11.79 | 18.21 | 0.32 | 0.41 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua methali iliyo sawa kimaana na methali isemayo “Ngoma ikilia sana hupasuka.” Watahiniwa 343,108 sawa na asilimia 43.33 walichagua A “Mgema akisifiwa tembo hulitia maji” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 121,155 sawa na asilimia 15.3 waliochagua C “Tamaa mbele mauti nyuma” ambalo sio jibu sahihi hawakuwa na uelewa wa methali hiyo. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa maana ya methali hiyo ambayo hutumiwa kama funzo ni kwamba tamaa isiyokuwa na mipaka huweza kusababisha madhara makubwa na hata kifo. Aidha,

watahiniwa 84,266 sawa na asilimia 10.64 walichagua kipotoshi B "Debe tupu haliachi kutika" ambalo sio jibu sahihi kwa kuwa debe lisilokuwa na chochote ndani huwa linapiga kelele na kutikisika, hivyo kuwa tofauti na methali iliyotolewa.

Watahiniwa 237,612 sawa na asilimia 30 walichagua kati ya vipotoshi D "Mpanda ovyo, ndiye hula ovyo" ikiwa na maana kwamba ili kupata mafanikio maishani lazima kufanya kazi kwa bidii na juhudi kubwa, E "Mshindo mkuu huvuma mbali" ikiwa na maana jambo lolote ambalo limewagusa wengi hufahamika sehemu kubwa. Hivyo, kufanya methali hizo kutofautiana na methali iliyotolewa ambayo watahiniwa wangeweza kuilinganisha kwa usahihi kwa kuwa methali hizo hutumika mara kwa mara katika jamii.

**Swali la 24:** "Ukukuu wa kamba si upya wa ukambaa." Methali hii ina maana sawa na methali ipi?

A. Heri nusu shari kuliko shari kamili
B. Ukipata chungu kipya usitupe cha zamani
C. Kamba hukatikia pabovu
D. Nazi mbovu harabu ya nzima
E. Badiliko kwa mjukuu uanze na babu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 135,780 | 395,283 | 102,801 | 96,543 | 55,753 | 3,406 | 2,366 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 17.15 | 49.91 | 12.98 | 12.19 | 7.04 | 0.43 | 0.3 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua methali iliyo sawa kimaana na methali isemayo "Ukukuu wa kamba si upya wa ukambaa." Watahiniwa 395,283 sawa na asilimia 49.91 walichagua B

“Ukipata chungu kipya usitupe cha zamani” ambalo ndilo jibu sahihi ikiwa na maana kuwa usidharau kitu kwa kuwa tu ni cha zamani kwani huweza kuwa imara kuliko kilicho kipya. Watahiniwa 135,780 sawa na asilimia 17.15 walichagua A “Heri ya nusu shari kuliko shari kamili” ambacho sio jibu sahihi. Methali hiyo maana yake ni kuwa afadhali kupata japo kidogo kuliko kuharibikiwa na jambo lote. Aidha, watahiniwa 102,801 sawa na asilimia 12.98 waliochagua kipotoshi C “Kamba hukatikia pabovu” hawakuwa wanaelewa maana ya methali hii kuwa jambo liharibikapo anayelaumiwa ni yule ambaye ni mnyonge hata kama hakuwa na hatia.

Watahiniwa 152,296 sawa na asilimia 19.23 walichagua vipotoshi kati ya D “Nazi mbovu, harabu ya nzima” ikiwa na maana nazi moja mbovu huweza kuziharibu nazi zingine zilizowekwa pamoja nayo na E “Badiliko kwa mjukuu uanze na babu” ikiwa na maana hakuna mabadiliko yanayotokea ghafla bali yanafanyiwa kazi mapema. Hali hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana za methali hizo ambazo zina maana tofauti na ile ya “Ukukuu wa kamba si upya wa ukambaa.”

**Swali la 25:** “Hamadi kibindoni.” Kati ya tafsiri zifuatazo ni ipi inayotoa maana sahihi ya msemo huo?

A. Akiba ni ile iliyo nyingi
B. Weka akiba yako vizuri
C. Kizuri hakina budi kuhifadhiwa
D. Kikufaacho ni kile ulicho nacho
E. Akiba iliyohifadhiwa hunusurika.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 56,135 | 178,443 | 113,226 | 352,030 | 86,027 | 3,568 | 2,503 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 7.09 | 22.53 | 14.3 | 44.45 | 10.86 | 0.45 | 0.32 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa kutambua tafsiri inayotoa maana iliyo sawa na maana ya msemo "Hamadi kibindoni." Watahiniwa 352,030 sawa na asilimia 44.45 walichagua jibu sahihi D "Kikufaacho ni kile ulicho nacho." Msemo huu unasisitiza jamii kujiwekea akiba kwani pale itakapotokea shida kitakachomsaidia ni ile akiba aliyoweka. Uchaguzi wa kipotoshi B "Weka akiba yako vizuri" kwa watahiniwa 178,443 ambao ni sawa na asilimia 22.53 unaonesha kuwa watahiniwa hao walivutiwa na neno "kibindoni" ambalo lina maana mahali pa kuhifadhia fedha bila ya kuelewa maana hasa ya msemo huo. Watahiniwa 199,253 ambao ni sawa na asilimia 25.16 waliochagua vipotoshi kati ya C "Kizuri hakina budi kuhifadhiwa" na E "Akiba iliyohifadhiwa hunusurika" ambavyo havikuwa majibu sahihi kunaonesha kuwa watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa kimsingi vipotoshi hivyo vilikuwa na maana moja ya kuhifadhi akiba lakini havikufafanua kama akiba hiyo itamsaidiaje mtunzaji jambo ambalo ndiyo maana ya msemo " Hamadi kibindoni."

Uteuzi wa kipotoshi A "Akiba ni ile iliyo nyingi" kilichochaguliwa na watahihiwa 56, 135 ambao ni sawa na asilimia 7.09 ambacho sio jibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana ya msemo waliopewa ambao maana yake inasisitiza kuwa akiba ni akiba hata ikiwa kidogo kwa vile akiba hiyo inayokuwa kibindoni sio lazima iwe nyingi ili iweze kumsaidia mtu.

**Swali la 26:** "Samaki mkunje angali mbichi." Methali ipi kati ya zifuatazo ina maana sawa na hiyo?

A. Samaki huanza kuoza kichwani
B. Ukitaka riba sikio ziba
C. Jino la pembe si dawa ya pengo
D. Sikio la kufa halisikii dawa
E. Ngozi ivute ili maji.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 92,496 | 93,104 | 127,593 | 288,166 | 184,271 | 3,565 | 2,737 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.68 | 11.76 | 16.11 | 36.39 | 23.27 | 0.45 | 0.35 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa kubaini maana za methali za Kiswahili. Watahiniwa 184,271 sawa na asilimia 23.27 walichagua jibu sahihi ambalo ni E "Ngozi ivute ili maji" methali yenye maana kuwa rekebisha jambo mapema kabla halijaharibika sana, maana ambayo ni sawa na maana ya methali isemayo "Samaki mkunje angali mbichi." Watahiniwa 288,166 sawa na asilimia 36.39 walichagua kipotoshi D "Sikio la kufa halisikii dawa" jibu ambalo si sahihi, kwani methali hii maana yake ni kuwa jambo ambalo limekwishaharibika hata ufanye juhudi kiasi gani haliwezi kamwe kuwa zuri. Watahiniwa 313,193 sawa na asilimia 39.55 walichagua vipotoshi kati ya A, B na C ambavyo si majibu sahihi. Kipotoshi A "Samaki huanza kuoza kichwani" maana yake ni kwamba jambo linapoharibika katika jamii huanzia kwa viongozi, kipotoshi B "Ukitaka riba sikio ziba" maana yake ni kuwa unapotaka mafanikio katika jambo lolote usihofie maneno au lawama za watu na kipotoshi C "Jino

la pembe si dawa ya pengo" maana yake ni kwamba upatapo kitu kipya baada ya kupotelewa na cha zamani hicho kipya hakiwezi kuwa sawa na cha zamani. Watahiniwa walioshindwa kuchagua jibu sahihi wanadhihirisha kuwa hawana uelewa wa kutosha kuhusu maana za methali za Kiswahili. Swali hilo lilitarajiwa kuwa miongoni mwa maswali ambayo watahiniwa wangeweza kujibu kwa usahihi kwani methali hiyo hutumika mara kwa mara katika jamii.

**Swali la 27:** Methali isemayo, "Chanda chema huvikwa pete" inatoa funzo gani?

A. Dhahabu hupewa aliyeshinda
B. Jambo zuri huzawadiwa
C. Inapobidi jamii hupewa zawadi
D. Mtu mzuri husifiwa
E. Mshindi hupokea baraka.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 122,310 | 326,255 | 63,630 | 181,406 | 92,479 | 3,230 | 2,622 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.44 | 41.2 | 8.03 | 22.91 | 11.68 | 0.41 | 0.33 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa kuhusu tathmini ya methali aliyopewa. Mtahiniwa alitakiwa kueleza funzo linalopatikana katika methali isemayo "Chanda chema huvikwa pete." Watahiniwa 326,255 sawa na asilimia 41.2 walichagua jibu sahihi ambalo ni B "Jambo zuri huzawadiwa." Watahiniwa 459,825 sawa na asilimia 58.06 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A, C, D na E kwa kuwa hawakuwa na uwezo wa kutosha katika kutathmini funzo linalopatikana katika methali waliyoulizwa.

**Swali la 28:** “Ukitaka kuruka agana na nyonga.” Methali hii inaasa kuhusu jambo gani?

A. Tekeleza jambo kwa kufuata maelekezo

B. Tafakari kwa kina kabla ya kutenda

C. Fuatilia kwa haraka, ndipo utende

D. Kuuliza ni muhimu kabla ya kutenda

E. Tenda jambo kwa kufanya maamuzi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 125,264 | 402,776 | 62,804 | 124,614 | 70,698 | 3,300 | 2,476 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.82 | 50.86 | 7.93 | 15.74 | 8.93 | 0.42 | 0.31 |

Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu semi za Kiswahili na hasa methali. Watahiniwa 402,776 sawa na asilimia 50.86 ya watahiniwa waliofanya mtihani walichagua chaguo B “Tafakari kwa kina kabla ya kutenda” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 383,380 sawa na asilimia 48.42 ya watahiniwa walichagua kati ya vipotoshi A, C, D na E kwa kuwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu methali na hususan methali waliyoulizwa katika swali hilo.

**Swali la 29:** Methali isemayo, “Mpofuka ukongweni ______________” hukamilishwa na kifungu kipi cha maneno kati ya hivi vifuatavyo?

A. huzuni yake ni kubwa

B. hakumbuki zamani

C. hupotea njia

D. hukumbuka ujanani

E. hapotewi na njia.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 78,096 | 100,976 | 141,683 | 201,966 | 262,222 | 4,025 | 2,964 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.86 | 12.75 | 17.89 | 25.5 | 33.11 | 0.51 | 0.37 |

Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu muundo wa methali za Kiswahili. Mtahiniwa alitakiwa kukamilisha methali aliyopewa kwa kuchagua kifungu cha maneno kinachokamilisha tungo aliyopewa ili kuunda methali inayoleta maana. Watahiniwa 262,222 sawa na asilimia 33.11 ya watahiniwa ndio waliochagua jibu sahihi ambalo ni E "hapotewi na njia" jibu linaloikamilisha methali hiyo na kuifanya iwe na maana kuwa; mtu aliyezoea jambo fulani na ambalo amelifanya kwa muda mrefu, hupata ujuzi wa kutosha hivyo hawezi kusumbuka wakati mwingine atakapofanya jambo hilo hilo, kwa kuwa amekwishalizoea. Aidha, watahiniwa 522,721 sawa na asilimia 66 walichagua kati ya kipotoshi A, B, C na D jambo linaloonesha kuwa watahiniwa hao hawana ujuzi wa kutosha kuhusu muundo wa methali za Kiswahili.

**Swali la 30:** Nikikutana na adui yangu nanyongea. Jibu la kitendawili hiki ni lipi?

A. Askari

B. Ugonjwa

C. Mbwa

D. Ujinga

E. Umaskini.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 60,543 | 590,990 | 59,962 | 32026 | 43,287 | 2,685 | 2,439 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 7.64 | 74.63 | 7.57 | 4.04 | 5.47 | 0.34 | 0.31 |

Swali lililenga kupima tanzu za semi za Kiswahili hasa vitendawili. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa kwa usahihi na watahiniwa wengi. Watahiniwa 590,990 sawa na asilimia 74.63 walichagua chaguo B “Ugonjwa” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 195,818 sawa na asilimia 24.72 walichagua kati ya vipotoshi A, C, D na E ambavyo sio majibu sahihi. Vipotoshi “askari,” “mbwa,” “ujinga” na “umaskini” ni maadui ambao watu huweza kupambana nao kwa kila hali na hasa mtu akiwa na nguvu zake. Aidha, vipotoshi hivyo ni tofauti na “ugonjwa” kwani haujali hali yoyote aliyo nayo mtu. Ugonjwa umpatapo yeyote hunyong’onyea hata akiwa mkali kama mbwa, maskini au mjinga na hata akiwa ni askari ambaye hujilinda kwa kutumia silaha.

## 2.3 Sehemu C: Ufahamu

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyotokana na kifungu hicho. Kifungu walichopewa kilisomeka kama ifuatavyo:

*Mabadiliko ya hali ya hewa yamekuwa makubwa kiasi cha kutisha. Zamani mababu zetu walitabiri mvua wao wenyewe pasi na kuwa na vyombo vya kisasa. Suala linalozungumziwa sana siku hizi ni mabadiliko ya hali ya hewa na athari zake kwa jamii nzima. Kila mtu*

*ana wasiwasi kuhusu mvua ambazo huchukua muda mrefu bila kunyesha.*

*Ukosefu wa mvua ambao mwishowe huleta ukame na njaa umechangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu ambazo zinaongezeka kwa haraka siku hadi siku. Shughuli hizo mbalimbali ambazo kwa upande mmoja zinaonekana kama za kimaendeleo ni kuongezeka kwa matumizi ya maliasili. Mifano mbalimbali ambayo inaonesha matumizi hayo ni pamoja na ujenzi wa nyumba nyingi zaidi, kupata nishati ya kutosha kwa ajili ya kupikia na upatikanaji wa mbao na magogo kwa wingi kwa matumizi ya ndani na hata ya nje ya nchi.*

*Hata hivyo, ili maendeleo hayo yawe na mwelekeo chanya jamii inalazimika kupanda miti kwa wingi ili kukidhi mahitaji hayo. Aidha, ni vema kuzingatia kuwa ukataji miti ni chanzo kikubwa cha mito na vijito kuwa na maji haba au kukauka kabisa.*

**Swali la 31:** Kichwa cha habari kinachofaa kwa habari hii ni kipi?

A. Mabadiliko ya hali ya hewa

B. Ukosefu wa chakula

C. Kuongezeka kwa joto

D. Kuongezeka kwa ukame

E. Mabadiliko na athari zake.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 585,413 | 50,842 | 38,229 | 48,695 | 63,653 | 2,366 | 2,734 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 73.92 | 6.42 | 4.83 | 6.15 | 8.04 | 0.3 | 0.35 |

Swali liliwapima watahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui ya habari waliyoisoma. Watahiniwa 585,413 sawa na asilimia 73.92 walijibu swali vizuri na kwa usahihi kwani waliweza kubaini kichwa cha habari kuwa ni A "Mabadiliko ya hali ya hewa." Watahiniwa 201,419 ambao ni sawa na asilimia 25.44 walichagua kati ya vipotoshi B, C, D na E yaani "Ukosefu wa chakula," "Kuongezeka kwa joto," "Kuongezeka kwa ukame" na "Mabadiliko na athari zake" ambavyo havikuwa majibu sahihi kwavile ni mambo ambayo yamejumuishwa ndani ya jibu sahihi

**Swali 32:** Tatizo kubwa zaidi ambalo husababishwa na ukosefu wa mvua kwa muda mrefu ni lipi kati ya haya yafuatayo?

A. Kukatika kwa umeme
B. Ujenzi kupungua
C. Kukosekana nishati
D. Kukosekana kwa miti
E. Kuwepo kwa baa la njaa.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 43,287 | 59,961 | 85,212 | 357,864 | 239,274 | 3,057 | 3,277 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 5.47 | 7.57 | 10.76 | 45.19 | 30.21 | 0.39 | 0.41 |

Swali lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa katika kutambua mawazo makuu yaliyomo katika kifungu cha habari alichopewa. Watahiniwa

357,864 sawa na asilimia 45.19 ya watahiniwa walichagua kipotoshi D "Kukosekana kwa miti" Jibu hilo si sahihi kwa sababu kukosekana kwa miti si tatizo kubwa linalotokana na kukosekana kwa mvua kwa muda mrefu. Aidha, miti inapokosekana kuna vitu/malighafi ambazo unaweza kuzitumia kama mbadala. Watahiniwa 239,274 sawa na asilimia 30.21 tu ya watahiniwa waliofanya mtihani ndiyo waliochagua jibu sahihi E "Kuwepo kwa baa la njaa," kuwa hilo ni tatizo kubwa kwa sababu linaigharimu nchi na huweza kusababisha vifo. Aidha, watahiniwa 188,460 sawa na asilimia 23.8 walichagua kati ya vipotoshi A, B na C ambavyo si majibu sahihi kwa sababu si matatizo yanayohusiana na kukosekana kwa mvua. Uteuzi wa vipotoshi visivyo sahihi unadhihirisha kuwa watahiniwa hawana uwezo wa kusoma kifungu cha habari na kutoa tathmini iliyo sahihi.

**Swali la 33**: Mwandishi anayaelezea mabadiliko ya hali ya hewa kuwa yalikuwa

A. hayakadiriki
B. ya hali ya juu
C. ya kutisha
D. ya kukadirika
E. hayatabiriki.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 74,885 | 121,979 | 300,438 | 114,285 | 174,627 | 3,313 | 2,405 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 9.46 | 15.4 | 37.94 | 14.43 | 22.05 | 0.42 | 0.3 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kusoma kwa makini kifungu cha habari na kutambua mambo muhimu yaliyoelezwa.

Watahiniwa 300,438 sawa na asilimia 37.94 ya watahiniwa waliofanya mtihani waliweza kujibu swali hili kwa usahihi kwa kuchagua jibu C “ya kutisha.” Watahiniwa hao waliweza kujibu kwa usahihi kwa sababu waliweza kurejea aya ya kwanza ambayo ilikuwa inaelezea kuhusu hali ya mabadiliko hayo. Watahiniwa waliochagua vipotoshi A “hayakadiriki” B “ya hali ya juu,” D “ya kukadirika” na E “hayatabiriki” walikuwa 485,776 sawa na asilimia 61.34. Watahiniwa hao walikosa ujuzi wa kusoma kwa makini na kupata ufahamu kutoka katika kifungu walichopewa. Aidha, watahiniwa hao walishindwa kuhawilisha maarifa katika hoja iliyopo katika mstari wa kwanza wa aya ya kwanza.

**Swali la 34:** Neno “haba” kama lilivyotumika katika kifungu cha habari lina maana gani?

A. Kidogo
B. Kiasi
C. Kadri
D. Wastani
E. Rasharasha.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 482,033 | 107,572 | 67,313 | 60,279 | 70,386 | 2,426 | 1,923 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 60.87 | 13.58 | 8.5 | 7.61 | 8.89 | 0.31 | 0.24 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya watahiniwa kuhusu maana ya misamiati kama ilivyotumika katika kifungu cha habari walichopewa. Watahiniwa 482,033 sawa na asilimia 60.87 walijibu swali kwa usahihi kutokana na maarifa waliyokuwa nayo na hivyo walichagua jibu A “Kidogo” ambalo ndilo maana sahihi ya neno “haba.” Jumla ya watahiniwa 305,550 sawa na asilimia 38.58 walichagua vipotoshi B

“kiasi,” C “kadri” D “wastani” na E “rasharasha” ambavyo si majibu sahihi. Uteuzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kuwa watahiniwa hao walikosa maarifa ya kuwawezesha kufahamu maana za misamiati na hasa ikizingatiwa kuwa maneno hayo yanahusiana kwa kuwa yanahusisha idadi ingawa maana zake ni tofauti.

**Swali la 35:** Dalili mojawapo kubwa ya maendeleo ni ipi kama ilivyoelezwa katika kifungu cha habari?

A. Kupata nishati ya kupikia
B. Ongezeko la miti ya kujengea
C. Ongezeko la utumiaji wa maliasili
D. Upatikanaji wa mbao na magogo
E. Ongezeko la ujenzi wa nyumba.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C*** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 121,217 | 103,967 | 296,244 | 137,819 | 128,919 | 2,017 | 1,749 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 15.31 | 13.13 | 37.41 | 17.4 | 16.28 | 0.25 | 0.22 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa watahiniwa katika kusoma na kuelewa yatokanayo na habari waliyosoma. Watahiniwa 296,244 sawa na asilimia 37.41 walielewa habari na kuweza kuchagua jibu sahihi C “Ongezeko la utumiaji wa maliasili.” Watahiniwa hao pia waliweza kuhawilisha maarifa yaliyomo katika kifungu cha habari hususan katika aya ya pili mstari wa nne ambao unaelezea matumizi ya maliasili. Uteuzi wa kipotoshi B “ongezeko la miti ya kujengea” uliofanywa na watahiniwa 103,967 sawa na asilimia 13.13 ulisababishwa na watahiniwa hao kuhusisha miti na malighafi muhimu ya ujenzi. Inawezekana watahiniwa walichagua kipotoshi hicho kwa

sababu watanzania wengi wanaishi vijijini ambako miti hutumika kujengea nyumba. Hata hivyo, matumizi ya miti katika ujenzi hayawezi kuleta maendeleo, kwa sababu huhusisha uharibifu wa mazingira kwa tendo la kukata miti. Aidha, uteuzi wa vipotoshi kati ya A, D na E ambayo si majibu sahihi uliofanywa na watahiniwa 387,955 sawa na asilimia 48.99, ulionekana kuwavutia watahiniwa hao kwa sababu vipotoshi hivyo vilitajwa katika kifungu cha habari kama mifano ya matumizi ya maliasili na si shughuli za kimaendeleo.

**Swali la 36:** Mabadiliko ya hali ya hewa yana maana sawa na ipi kati ya hizi zifuatazo?

A. Uoto
B. Jotoridi
C. Mazingira ya nchi
D. Sura ya nchi
E. Tabia nchi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 90,024 | 110,004 | 143,600 | 121,846 | 321,287 | 2,928 | 2,243 |
| Asilimia ya watahiniwa | 11.37 | 13.89 | 18.13 | 15.3 | 40.57 | 0.37 | 0.28 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika matumizi ya sinonimu katika lugha ya Kiswahili. Watahiniwa 321,287 sawa na asilimia 40.57 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu E “Tabia nchi” ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa hao walikuwa wanajua neno lenye maana sawa na mabadiliko ya hali ya hewa. Hii inawezekana ni kwa sababu wamekuwa wakifuatilia mambo mtambuka yanayozungumzwa mara nyingi kwenye vyombo vya habari ikiwemo mikutano mikubwa inayofanyika ulimwenguni kuhusu

suala zima la mazingira. Watahiniwa 465,474 ambao ni sawa na asilimia 58.69 walichagua kati ya vipotoshi A, B, C na D ambayo si majibu sahihi kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu neno lenye maana sawa na mabadiliko ya hali ya hewa.

**Swali la 37:** Kisawe cha neno "mwishowe" kama kilivyotumika katika habari hii ni kipi?

A. Tamati
B. Hatima
C. Baadaye
D. Hatimaye
E. Hitimisho.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D* | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 200,031 | 59,384 | 108,919 | 273,502 | 144,043 | 3,302 | 2,751 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 25.26 | 7.5 | 13.75 | 34.54 | 18.19 | 0.42 | 0.35 |

Swali lililenga kupima uelewa wa mtahiniwa kuhusu visawe vya maneno ya Kiswahili. Watahiniwa 273,502 sawa na asilimia 34.54 ya watahiniwa walichagua jibu D "Hatimaye" ambalo ndilo jibu sahihi. Watahiniwa 512,377 sawa na asilimia 64.7 walichagua kati ya kipotoshi A, B, C na E ambavyo sio majibu sahihi, hali inayoonesha kuwa ama hawakuelewa matakwa ya swali au hawakuwa na uelewa unaotakiwa wa visawe sahihi vya maneno. Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kuelewa maana ya neno "mwishowe" ili kuweza kupata kisawe sahihi.

**Swali la 38:** Watu wa zamani waliweza kutabiri mvua kwa kutumia

A. vyombo vya kisasa

B. kipaji chao wenyewe

C. vyombo vya zamani

D. kipima mvua cha kienyeji

E. ubunifu waliorithi.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 234,888 | 273,842 | 90,339 | 77,856 | 109,596 | 2,831 | 2,580 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 29.66 | 34.58 | 11.41 | 9.83 | 13.84 | 0.36 | 0.33 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kusoma na kuelewa maudhui yaliyomo katika kifungu cha habari alichopewa. Watahiniwa 273,842 sawa na asilimia 34.58 walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu B "kipaji chao wenyewe." Watahiniwa hao waliweza kuhusisha hali ya utabiri wa mvua uliofanywa na mababu zao wenyewe pasi na vyombo vya kisasa kuwa hicho kilikuwa ni kipaji chao. Kipotoshi A "vyombo vya kisasa" kilichaguliwa na watahiniwa 234,888 sawa na asilimia 29.66 ambayo ni kubwa zaidi kuliko vipotoshi vingine vyote. Hali hii huenda ilisababishwa na kuvutiwa na maneno "vyombo vya kisasa" ambayo yamo katika aya ya kwanza ya kifungu walichopewa. Aidha, yawezekana kuwa hawajui maana ya maneno 'pasi na' ambayo yanamaanisha 'bila kuwa na' huenda walidhani yanamaanisha "kwa kutumia." Uteuzi wa vipotoshi C, D na E ambavyo havikuwa majibu sahihi ulifanywa na watahiniwa 277,791 sawa na asilimia 35.08 kutokana na uwezo mdogo wa kubaini mawazo yaliyomo katika kifungu cha habari.

**Swali la 39:** Mito na vijito huwa na maji haba au kukauka kutokana na nini?

A. Kukata miti kwa wingi

B. Kuchoma majani karibu na mito

C. Kukata majani kwa wingi

D. Kuchoma miti iliyozunguka mito

E. Kukata miti iliyozunguka vijito.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 458,670 | 59,404 | 54,477 | 93,744 | 119,510 | 3,431 | 2,696 |
| Asilimia ya watahiniwa | 57.92 | 7.5 | 6.88 | 11.84 | 15.09 | 0.43 | 0.34 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa wa kusoma na kuelewa kifungu cha habari alichopewa. Watahiniwa 458,670 sawa na asilimia 57.92 walijibu swali kwa usahihi kwa kubaini jibu sahihi ambalo ni A "Kukata miti kwa wingi." Uteuzi huo unaonesha kuwa licha ya watahiniwa kusoma na kuelewa kifungu cha habari walichopewa pia wana ufahamu wa kutosha kuhusu athari za kimazingira zinazotokana na tendo la ukataji wa miti ovyo, ambapo husababisha kukosekana kwa mvua na hatimaye mito na vijito vinakosa maji. Aidha, watahiniwa 327,135 sawa na asilimia 41.31 waliochagua vipotoshi B, C, D na E walikosa uelewa utokanao na usomaji wa habari kwa makini.

**Swali la 40**: Nishati ni neno lenye maana sawa na lipi?

A. Kawa

B. Kivo

C. Kiwi

D. Kivi

E. Kawi.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C | D | E* | Wasiojibu | Nyingine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 181,337 | 160,019 | 197,812 | 121,489 | 120,589 | 8,089 | 2,597 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 22.9 | 20.21 | 24.98 | 15.34 | 15.23 | 1.02 | 0.33 |

Swali lililenga kupima ujuzi wa mtahiniwa katika kutumia msamiati. Hili ni swali lililojibiwa vibaya kuliko maswali mengine yote katika mtihani huu kwani ni watahiniwa 120,589 tu sawa na asilimia 15.23 ndio waliochagua jibu sahihi E "kawi" lenye maana ya nishati. Asilimia 24.98 walichagua kipotoshi C "kiwi" lenye maana zifuatazo; komeo, matatizo ya kuona, tabia mbaya ya uroho na wino mweusi wa ngisi anaotoa ili kujikinga na adui zake. Asilimia 22.9 walichagua kipotoshi A "kawa" lenye maana ya kitu kilichoshonwa kwa ukili uliosukwa kwa chane za ukindu kitumiwacho kama pambo la nyumbani au kufunikia chakula. Asilimia 20.21 walichagua kipotoshi B "kivo" neno lenye maana ya kitu kilichozidi kiasi kinachotakiwa, pia ni kifuu cha nazi. Aidha, asilimia 15.34 walichagua kipotoshi D "kivi" lenye maana ya kiwiko na pia ni wino wa ngisi. Uteuzi wa vipotoshi kati ya A, B, C au D ambavyo si majibu sahihi unaonesha wazi kuwa watahiniwa hao 660,657 ambao sawa na asilimia 83.43 hawana ujuzi wa kutosha kuhusu maana za misamiati ya Kiswahili.

## 2.4 Sehemu D: Ushairi

Katika sehemu hii watahiniwa walitakiwa kusoma shairi lifuatalo na kujibu maswali yanayotokana na shairi hilo.

*Msituni nikakuta, nyuki wamo mzingani,*
*Kwa juhudi wanakita, mara nje mara ndani,*
*Husuda wameikata, hata hawasengenyani,*
*Nyuki ni wadudu duni, wanashinda kwa umoja.*

*Mchwa nao nikaona, wamejenga maskani,*
*Wafanya bidii sana, uvivu hawatamani,*
*Wao husaidiana, tena hawadanganyani,*
*Mchwa wadudu wa chini, wanaishi kwa umoja.*

*Nalo jeshi la siafu, hutandawaa njiani,*
*Laenda bila ya hofu, maana lajiamini,*
*Silaha zao dhaifu, meno tena hawaoni,*
*Wa kuwatadia nani, kwani wanao umoja.*

*Nao chungu wachukuzi, nyamarima wa njiani,*
*Maskini wapagazi, mizigo yao kichwani,*
*Ingawa si wachokozi, wakali ukiwahini,*
*Katu hawafarakani, wanadumu kwa umoja.*

**Swali la 41:** Mwandishi wa shairi hili anasisitiza kuhusu nini?

A. Uzalishaji

B. Maarifa

C. Ushirikiano

D. Urafiki

E. Undugu.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 65,392 | 62,449 | 565,612 | 53,109 | 39,568 | 3,690 | 2,112 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 8.26 | 7.89 | 71.42 | 6.71 | 5 | 0.47 | 0.27 |

Swali lilikuwa linawapima watahiniwa kuhusu uelewa wa maudhui na ujumbe wa shairi kwa ujumla na ni swali lililojibiwa vizuri katika mada hii. Watahiniwa 565,612 sawa na asilimia 71.42 walijibu swali kwa usahihi kwa kubaini jibu sahihi kuwa ni C “Ushirikiano.” Watahiniwa 220,518 sawa na asilimia 27.86 waliochagua vipotoshi kati ya A, B, D na E walikosa uelewa utokanao na usomaji wa shairi kwa makini, kwa

sababu kuwa na uzalishaji, maarifa, urafiki na undugu hakuwezi kuleta mafanikio endapo hakuna ushirikiano. Uzalishaji unaweza kufanywa na mtu mmoja kwa manufaa yake, mtu anaweza kuwa na maarifa akabaki nayo bila kuyatumia, watu wanaweza kujenga urafiki lakini si lazima marafiki kushirikiana katika jambo/mambo mbalimbali. Hali kadhalika, undugu hauwafanyi watu kuwa na ushirikiano. Hivyo mshairi anasisitiza watu kushirikiana katika jamii ili kuleta maendeleo na hata amani kwa kuwa maadui hawatakuwa na nafasi ya kuwashinda kwa urahisi.

**Swali la 42:** Shairi hili lina mizani ngapi kwa kila mstari?

A. Sita
B. Kumi na sita
C. Tano
D. Saba
E. Thelathini na moja.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A | B* | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 50,525 | 575,835 | 69,187 | 49,358 | 41,879 | 2,903 | 2,245 |
| Asilimia ya watahiniwa | 6.38 | 72.71 | 8.74 | 6.23 | 5.2 | 0.37 | 0.28 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi. Swali lilijibiwa kwa usahihi na zaidi ya nusu ya watahiniwa, kwani watahiniwa 575,835 sawa na asilimia 72.71 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi ambalo ni B “Kumi na sita.” Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utunzi wa mashairi hasa dhana ya mizani. Watahiniwa 50,525 sawa na asilimia 6.38 walichagua kipotoshi A “Sita” kwa kuwa walihusisha idadi ya maneno katika ubeti wa 3 ambao kila mstari una maneno sita, hali ambayo

haijitokezi katika beti zingine za shairi hilo. Watahiniwa 69,187 sawa na asilimia 8.74 walichagua kipotoshi C “Tano” kwa kuwa walivutiwa na mstari wa kwanza wa ubeti wa kwanza ambao una idadi ya maneno matano. Aidha, uteuzi wa kipotoshi D “Saba” uliofanywa na watahiniwa 49,358 sawa na asilimia 6.23 unaonesha kuwa watahiniwa walivutiwa na mstari wa mwisho wa ubeti wa kwanza na ubeti wa mwisho wa ubeti wa pili, kwa kuwa idadi ya maneno katika mistari hiyo ni saba. Hali kadhalika, watahiniwa 41,879 sawa na asilimia 5.2 waliteua kipotoshi E “Thelathini na moja” kwa vile walihusisha na idadi ya herufi/vitamkwa vilivyopo katika mstari wa kwanza wa ubeti wa pili. Kwa ujumla uteuzi wa vipotoshi ambavyo si majibu sahihi unaonesha wazi kuwa watahiniwa hao hawana ujuzi wa kutosha kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi.

**Swali la 43:** Neno “husuda” kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana gani?

A. Uhasama
B. Hisani
C. Hiana
D. Wivu
E. Huzuni.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D*** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 182,113 | 107,975 | 96,380 | 254,947 | 143,301 | 4,038 | 3,178 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 23 | 13.63 | 12.17 | 32.19 | 18.1 | 0.51 | 0.4 |

Swali lilikuwa linapima matumizi ya msamiati kama ulivyotumika katika shairi. Watahiniwa 254,947 sawa na asilimia 32.19 walijibu kwa

usahihi kwa kuchagua jibu D “Wivu” ambalo ndilo lilikuwa na maana sawa na neno “husuda.” Aidha, watahiniwa 529,769 sawa na asilimia 66.9 walichagua vipotoshi kati ya A, B, C na E, ambavyo sio majibu sahihi. Watahiniwa hao walishindwa kutofautisha maana ya neno husuda na maneno kama vile “uhasama” ambalo maana yake ni hali ya kufarakana kutokana na ugomvi, “Hisani” lenye maana ya moyo wa kumtendea mtu mazuri, wema au fadhila. Pia “Hiana” lenye maana ya kumnyima mtu mwingine asifaidike na ulichonacho au ni kutomfanyia mtu haki. Aidha, neno “Huzuni” lenye maana ya hali ya kuwa na masikitiko au majonzi. Kwa ujumla maneno yaliyomo katika vipotoshi A, B, C na E yana maana ambayo haihusiani kabisa na neno husuda.

**Swali la 44:** Kisawe cha neno “Tadi” ni kipi?

A. Uchokozi
B. Tishio
C. Kemea
D. Ukombozi
E. Umbua.

Majibu ya watahiniwa

| Chaguo | A* | B | C | D | E | Wasiojibu | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 258,938 | 244,700 | 113,793 | 112,700 | 52,869 | 6,439 | 2,493 |
| Asilimia ya watahiniwa | 32.7 | 30.9 | 14.37 | 14.23 | 6.68 | 0.81 | 0.31 |

Swali lilikuwa linapima matumizi ya visawe vya maneno ya Kiswahili. Watahiniwa 258,938 sawa na asilimia 32.7 ya watahiniwa walijibu kwa usahihi kwa kuchagua jibu A “Uchokozi” ambalo ndilo kisawe cha neno “tadi.” Aidha, watahiniwa 524,062 sawa na asilimia 66.18 walichagua vipotoshi kati ya B, C, D na E, kwa kuwa walishindwa

kutofautisha neno tadi lenye maana ya uchokozi na maana za maneno kama vile; “tishio” lenye maana ya jambo/hali inayomfanya mtu awe na wasiwasi wa usalama wa maisha yake au shughuli zake, “kemea” lenye maana ya kumpigia mtu kelele kwa hasira/gombeza, “ukombozi” lenye maana ya uokoaji wa watu kutoka kwenye hali mbaya ya udhalimu au hali duni na “umbua” lenye maana ya tendo la kumtoa mtu/kitu thamani yake. Kwa ujumla kushindwa kwa watahiniwa hao ni kutokana na kutokuelewa maana mbalimbali za maneno.

**Swali la 45:** Kina cha kati katika ubeti wa pili ni kipi?

A. Wa
B. Na
C. Ja
D. U
E. Ni.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B*** | **C** | **D** | **E** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 90,993 | 536,126 | 50,293 | 53,024 | 56,003 | 3,118 | 2,375 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 11.49 | 67.7 | 6.35 | 6.7 | 7.07 | 0.39 | 0.3 |

Swali lilikuwa linapima maarifa ya mtahiniwa kuhusu kanuni za utunzi wa shairi, hususan upangaji wa vina. Watahiniwa 536,126 sawa na asilimia ya 67.7 ya watahiniwa walijibu swali kwa usahihi kwa kuchagua jibu B **“**Na**”** kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya vina vya kati. Watahiniwa 250,313 sawa na asilimia 31.61 ya watahiniwa waliochagua vipotoshi kati ya A, C, D na E hawakubaini vina vya kati katika ubeti wa tatu wa shairi hili kwa kuwa hawana ujuzi wa kutosha kuhusu kanuni za utunzi wa mashairi. Kwa

mfano, walioteua kipotoshi A walivutiwa na mizani “Wa” iliyopo katika kipande cha pili cha mstari wa kwanza wa ubeti wa pili, C walivutiwa na mizani “Ja” iliyopo katika kipande cha pili cha mstari wa mwisho wa ubeti wa pili, D walivutiwa na mizani “U” iliyopo kwenye kipande cha pili cha mstari wa pili wa ubeti wa pili na E “Ni” walivutiwa na mizani ya mwisho ya kipande cha pili cha mstari wa kwanza hadi wa tatu wa ubeti wa pili. Kwa ujumla uteuzi wa vipotoshi visivyokuwa na majibu sahihi unaonesha kuwa watahiniwa hawana ujuzi wa kutosha kuhusu dhana ya vina katika utunzi wa mashairi.

**Swali la 46:** Kichwa cha habari kinachofaa kwa shairi hili ni kipi?

A. Upekee wa wadudu
B. Umuhimu wa wadudu
C. Uhatari wa wadudu
D. Uchunguzi wa wadudu
E. Umoja wa wadudu.

Majibu ya watahiniwa

| **Chaguo** | **A** | **B** | **C** | **D** | **E*** | **Wasiojibu** | **Mengine** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya watahiniwa** | 58,145 | 119,664 | 66,346 | 65,761 | 473,085 | 4,852 | 4,079 |
| **Asilimia ya watahiniwa** | 7.34 | 15.11 | 8.38 | 8.3 | 59.74 | 0.61 | 0.52 |

Swali lilikuwa linapima uwezo wa mtahiniwa katika kubaini maudhui ya shairi alilolisoma. Watahiniwa 473,085 sawa na asilimia 59.74 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walikuwa na uelewa wa maudhui yanayopatikana katika shairi hilo, hivyo waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo lilikuwa E “Umoja wa wadudu” kwani shairi hili linahimiza watu katika jamii kuwa na umoja. Watahiniwa 309,916 sawa na asilimia 39.13 waliochagua vipotoshi A, B, C na D, hawakuwa na uelewa wa

kutosha kuhusu fasihi, hasa namna ya kupata maudhui ya kazi za fasihi hususan maudhui ya shairi.

## 2.5 Sehemu E: Utungaji

Katika sehemu hii, watahiniwa walipewa habari yenye sentensi nne (4) zilizoandikwa bila mtiririko sahihi na walitakiwa wazipange sentensi hizo ili ziwe na mtiririko wenye mantiki kwa kuzipa herufi A, B, C na D.

**Swali la 47:** Kwa njia hii, vizazi vilivyofuata viliweza kujua uvumbuzi uliofanywa kabla yao.

**Swali la 48:** Jambo muhimu lililofanywa na mababu zetu ni kuhifadhi kumbukumbu za uvumbuzi wao kwa kuchora kila kifaa walichovumbua.

**Swali la 49:** Kwa kutumia vizazi vilivyotangulia, nasi pia tunaweza kuvumbua vitu vipya ambavyo vitaweza kutuletea maendeleo zaidi.

**Swali la 50:** Hivyo maisha ya binadamu yakaendelea kuwa bora na yenye manufaa kila siku.

Majibu ya watahiniwa

| Swali | Jibu sahihi | Idadi ya watahiniwa | Asimilia ya watahiniwa | % Wasiojibu | % Mengine | % Jibu E |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **47** | **B** | 310,901 | 39.26 | 0.38 | 0.29 | 3.32 |
| **48** | **A** | 479,546 | 60.55 | 0.29 | 0.32 | 2.79 |
| **49** | **C** | 244,170 | 30.83 | 0.29 | 0.28 | 3.33 |
| **50** | **D** | 394,444 | 49.81 | 0.21 | 0.24 | 5.63 |

Swali hili lililenga kupima uwezo wa watahiniwa katika upangaji wa mawazo katika mtiririko wenye mantiki. Watahiniwa 310,901 ambao ni asilimia 39.26 waliweza kuandika sentensi ya kwanza kwa usahihi

kama ilivyotakiwa. Hata hivyo asilimia iliongezeka katika upangaji wa sentensi ya pili kwani watahiniwa 479,546 sawa na asilimia 60.55 waliandika sentensi hiyo kwa usahihi. Katika kukamilisha sentensi mbili za mwisho idadi na asilimia ya watahiniwa ilipungua na kufikia watahiniwa 244,170 sawa na asilimia 30.83 kwa sentensi ya tatu na watahiniwa 394,444 sawa na asilimia 49.81 kwa sentensi ya nne. Asilimia 2.79 hadi 5.63 walijibu maswali haya kama yale ya kuchagua kwa kujaza kipengele E ambacho hakikuwepo katika sehemu hii ya mtihani. Watahiniwa hawa hawakuelewa maelekezo ya swali na pia inaelekea kuwa walikuwa wanachagua majibu bila kusoma kilichoandikwa kwani wangekuwa wanasoma wangebaini kuwa herufi E haikuwa miongoni mwa herufi walizopaswa kuziandika katika swali hilo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MBALIMBALI

Mtihani wa Kiswahili ulitahini mada tano ambazo ni Sarufi, Lugha ya Kifasihi, Ufahamu, Ushairi na Utungaji. Ufaulu katika mada hizo ulikuwa wa wastani. Hata hivyo, uchambuzi wa mada unaonesha kuwa katika kila mada kuna maswali yaliyojibiwa vibaya na idadi kubwa ya watahiniwa lakini pia yapo yaliyojibiwa vizuri na idadi kubwa ya watahiniwa. Maswali yaliyojibiwa vibaya ni kama vile, swali la 8 kutoka mada ya Sarufi ambapo ni asilimia 23.94 tu ya watahiniwa ndio walioweza kuchagua jibu sahihi. Aidha, swali la 26 kutoka mada ya Lugha ya Kifasihi lilijibiwa kwa usahihi na watahiniwa wachache (184,271) sawa na asilimia 23.27. Vile vile ufaulu mdogo ulijitokeza katika swali la 32 na 40 yaliyotoka katika mada ya Ufahamu, ambapo kwa swali la 32 watahiniwa 239,274 sawa na asilimia 30.21 ndio

waliochagua jibu sahihi na swali la 40 watahiniwa 120,589 sawa na asilimia 15.23 tu ndio waliojibu swali hilo kwa usahihi.

Hata hivyo, kwa upande wa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa ni swali la 4 na 16 kutoka katika mada ya Sarufi, ambapo kwa swali la 4 watahiniwa 615,386 sawa na asilimia 77.71 na kwa swali la 16 watahiniwa 605,370 sawa na asilimia 76.44 waliweza kuchagua majibu sahihi. Swali moja (swali la 30) kutoka katika mada ya Lugha ya Kifasihi pia lilijibiwa vizuri na watahiniwa 590,990 sawa na asilimia 74.63. Hali kadhalika, swali la 31 lililotoka katika mada ya Ufahamu lilijibiwa vizuri na watahiniwa 585,413 sawa na asilimia 73.92. Uchambuzi wa ufaulu wa watahiniwa kwa kila mada katika somo la Kiswahili umewasilishwa katika **Kiambatisho**.

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa namna watahiniwa walivyojibu maswali unaonesha changamoto mbalimbali ambazo watahiniwa walikumbana nazo walipokuwa wakifanya mtihani. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu kwa kila mada kimekuwa ni cha wastani kama kilivyokuwa kwa mwaka 2013. Hata hivyo, kiwango cha ufaulu kwa mwaka huu wastani wake umeongezeka kwa asilimia 20.32. Uchambuzi wa mada umebaini kuwa wastani wa ufaulu kwa mada umeongezeka isipokuwa mada ya Ufahamu umeshuka kwa asilimia 13.65 kutoka asilimia 55.97 hadi 42.32. Hii inaonesha kuwa juhudi zaidi zinahitajika katika ujifunzaji na ufundishaji wa mada ya Ufahamu. Aidha, kwa mada ya Ushairi wastani wa ufaulu umeongezeka kwa asilimia 13.71 yaani kutoka 42.37 hadi 56.08.

Kutokana na uchambuzi huu, inaonesha wazi kuwa suala la ujifunzaji na ufundishaji wa somo la Kiswahili kwa shule za msingi linatakiwa lifanyike kwa ukamilifu ili kuwawezesha wanafunzi kutumia Kiswahili fasaha. Kwa kupitia wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili, somo hili linatakiwa kupewa kipaumbele kwa kuwawezesha wanafunzi kupata maarifa ya kutosha kuhusu somo la Kiswahili ili waweze kukabiliana na changamoto mbalimbali za kitaaluma na za kimaisha kuhusiana na lugha ya Kiswahili.

Itambulike wazi kuwa Kiswahili ni lugha ya Taifa, ni sehemu ya utamaduni wa Mtanzania na ni lugha inayoziunganisha nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na pia hutumika kimataifa. Hivyo, ni vema juhudi endelevu za kuinua lugha hii zifanyike kuanzia shule za msingi hadi elimu ya juu. Kwa kufanya hivi, lugha hii ya Kiswahili itakuwa imetendewa haki na kupewa hadhi inayostahili katika Taifa hili.

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuwawezesha watahiniwa kupata maarifa na ujuzi wa kutosha na pia katika kuboresha matokeo yao katika mtihani wa Kiswahili mambo yafuatayo hayana budi kuzingatiwa:

(a) Mamlaka husika zihakikishe kuwa shule zote za msingi zinakuwa na vitabu vya kiada na vya ziada vya kutosha kwa ajili ya somo la Kiswahili.

(b) Walimu wanaofundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama ilivyoelekezwa katika muhtasari.

(c) Ili kupata ujifunzaji na ufundishaji wenye mafanikio, walimu wanatakiwa kutoa mazoezi ya kutosha kwa wanafunzi kuhusiana na mada mbalimbali wanazofundisha, ikiwa ni pamoja na kuwapa wanafunzi mrejeo wa matokeo ya mazoezi hayo kila mara.

(d) Wanafunzi wajengwe kifikra kuhusiana na umuhimu wa somo la Kiswahili katika maisha yao. Aidha, wahamasishwe kusoma matini mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kufanya uchambuzi ulio makini katika mada ya Ufahamu.

(e) Wanafunzi wahamasishwe katika kutumia Kiswahili sanifu katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuboresha misamiati na sarufi ya lugha ya Kiswahili kwa ujumla.

**KIAMBATISHO**

## ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA KATIKA SOMO LA KISWAHILI PSLE 2013 NA 2014

| NA | MADA | UFAULU KWA KILA SWALI 2013 | | WASTANI WA UFAULU 2013 | MAONI 2013 | UFAULU KWA KILA SWALI 2014 | | WASTANI WA UFAULU 2014 | MAONI 2014 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | | | NAMBA YA SWALI | ASILIMIA YA UFAULU | | |
| 1 | Sarufi | 1 | 37.62 | 47.91 | Wastani | 1 | 33.95 | 50.91 | Wastani |
| | | 2 | 45.27 | | | 2 | 43.92 | | |
| | | 3 | 46.67 | | | 3 | 72.98 | | |
| | | 4 | 50.06 | | | 4 | 77.71 | | |
| | | 5 | 47.28 | | | 5 | 63.31 | | |
| | | 6 | 39.99 | | | 6 | 43.08 | | |
| | | 7 | 77.77 | | | 7 | 35.18 | | |
| | | 8 | 49.33 | | | 8 | 23.94 | | |
| | | 9 | 67.64 | | | 9 | 57.23 | | |
| | | 10 | 32.21 | | | 10 | 72.22 | | |
| | | 11 | 28.57 | | | 11 | 39.79 | | |
| | | 12 | 71.56 | | | 12 | 46.07 | | |
| | | 13 | 64.96 | | | 13 | 63.32 | | |
| | | 14 | 55.79 | | | 14 | 52.83 | | |
| | | 15 | 43.91 | | | 15 | 68.03 | | |
| | | 16 | 19.45 | | | 16 | 76.44 | | |
| | | 17 | 46.75 | | | 17 | 34.51 | | |
| | | 18 | 55.69 | | | 18 | 31.52 | | |
| | | 19 | 28.76 | | | 19 | 50.21 | | |
| | | 20 | 48.81 | | | 20 | 31.91 | | |
| 2 | Lugha ya Kifasihi | 21 | 62.9 | 44.17 | Wastani | 21 | 34.16 | 45.8 | Wastani |
| | | 22 | 57.47 | | | 22 | 63.41 | | |
| | | 23 | 43.63 | | | 23 | 43.33 | | |
| | | 24 | 48.54 | | | 24 | 49.91 | | |
| | | 25 | 25.27 | | | 25 | 44.45 | | |
| | | 26 | 44.48 | | | 26 | 23.27 | | |
| | | 27 | 38.78 | | | 27 | 41.2 | | |
| | | 28 | 83.59 | | | 28 | 50.86 | | |
| | | 29 | 23.31 | | | 29 | 33.11 | | |
| | | 30 | 13.71 | | | 30 | 74.63 | | |
| 3 | Ufahamu | 31 | 80.27 | 55.97 | Wastani | 31 | 73.92 | 42.32 | Wastani |
| | | 32 | 55.33 | | | 32 | 30.21 | | |
| | | 33 | 65.94 | | | 33 | 37.94 | | |
| | | 34 | 31.86 | | | 34 | 60.87 | | |
| | | 35 | 61.79 | | | 35 | 37.41 | | |
| | | 36 | 80.17 | | | 36 | 40.57 | | |
| | | 37 | 72.46 | | | 37 | 34.54 | | |
| | | 38 | 45.22 | | | 38 | 34.58 | | |
| | | 39 | 54.39 | | | 39 | 57.92 | | |
| | | 40 | 12.28 | | | 40 | 15.23 | | |
| 4 | Ushairi | 41 | 41.75 | 42.37 | Wastani | 41 | 71.42 | 56.08 | Wastani |
| | | 42 | 68.89 | | | 42 | 72.71 | | |
| | | 43 | 40.83 | | | 43 | 32.19 | | |
| | | 44 | 22.88 | | | 44 | 32.7 | | |
| | | 45 | 57.89 | | | 45 | 67.7 | | |
| | | 46 | 22 | | | 46 | 59.74 | | |
| 5 | Utungaji | 47 | 41.1 | 43.13 | Wastani | 47 | 39.26 | 45.11 | Wastani |
| | | 48 | 35.55 | | | 48 | 60.55 | | |
| | | 49 | 35.04 | | | 49 | 30.83 | | |
| | | 50 | 60.81 | | | 50 | 49.81 | | |